

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 43 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** SEPTEMBER 2024

WAZIRI MCHENGERWA AKABIDHI MAGARI 10 TSC, 9 YAPELEKWA OFISI ZA WILAYA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa (katikati) akishirikiana na viongozi mbalimbali kukata utepe ikiwa ni ishara ya ugawaji wa magari 10 kwa Tume ya Utumishi wa walimu (TSC). Hafla hiyo imefanyika tarehe 11 Agosti, 2024 katika Ofisi za OR – TAMISEMI Mtumba jijini Dodoma.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania



[tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

KONGOLE KWA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KUIWEZESHA TSC NGAZI YA WILAYA KUPATA MAGARI

Tarehe 11 Agost, 2024 Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa alikabidhi magari 10 kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) huku magari tisa (9) yakipelekwa katika Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya.

Hii ni mara ya kwanza kwa Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya kupata magari ikiwa ni sehemu ya jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania za kufanya mageuzi makubwa katika Sekta ya Elimu na Walimu.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi magari hayo iliyofanyika tarehe 11 Agosti,

2024 katika Ofisi za TAMISEMI Mtumba jijini Dodoma, Waziri Mchengerwa alisema kuwa huo ni mwanzo wa kuhakikisha ofisi za Tume ngazi ya Wilaya zinakuwa na mazingira bora ya kuwafikia walimu na kuwapa huduma stahiki.

Ni wajibu wa watumishi ambao ofisi zao zimepata magari kuhakikisha magari hayo yanatunzwa vizuri na yanatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa ili kuweza kuongeza ufanisi na ubora wa elimu.

Matumaini yetu ni kuwa baada ya kupata magari hayo hakutakuwa na visingizio vya kushindwa kutembelea walimu katika kusikiliza na kutatua changamoto zao badala ya kuwasubiri wafuate huduma ofisini.

BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Paulina M. Nkwama

Wajumbe

Richard L. Odongo
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya

Mhariri Mkuu

Artemony T. Vincent


Mhariri

Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa

Lucas G. Ogunde

KATUNI



Wasiliana nasi kwa Simu: +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**

WAZIRI MCHENGERWA AKABIDHI MAGARI 10 TSC, 9 YAPELEKWA OFISI ZA WILAYA

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa amekabidhi magari 10 kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) huku magari tisa (9) yakipelekwa katika Ofisi za TSC ngazi ya Wilaya.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi magari hayo iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 katika Ofisi za TAMISEMI Mtumba jijini Dodoma, Waziri Mchengerwa alisema kuwa Serikali inatambua kuwepo kwa uhitaji mkubwa wa magari katika Ofisi za TSC 139 zilizopo katika kila wilaya nchini.

Alisema kuwa magari 10 yaliyotolewa ni mwanzo wa kuanza kuboresha mazingira ya utendaji kwa Makatibu Wasaidizi ili waweze kutekeleza mjukumu yao kwa ufanisi.

“Ikumbukwe kuwa Serikali imeshatoa magari kwa Makatibu Tawala Wasaidizi Seksheni ya Elimu wote nchini, Wakuu wa Divisheni za Elimu Msingi na Sekondari wote na sasa tumeanza kwa Makatibu Wasaidizi wa TSC wa Wilaya,” alisema.

Alisema lengo la kutoa magari hayo ni kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za elimu zinazofanyika katika ngazi ya shule pamoja na kuwafikia walimu katika vituo vyao ili kuwasilikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili.

Mhe. Mchengerwa alisema kuwa jukumu la usimamizi wa Elimu linahitaji uwajibikaji na usimamizi thabiti katika ngazi ya Taifa, Mikoa, Halmashauri, Kata na Shule.

Alisema kuwa pamoja na bidii, weledi, ubunifu, uaminifu na utiifu, mafanikio katika usimamizi



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa akitoa hotuba wakati wa hafla ya kukabidhi magari kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 Mtumba jijini Dodoma.

wa elimu yanategemea pia uwezeshwaji wa vifaa na vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri.

Mhe. Mchengerwa aliongeza kuwa matarajio ya Serikali ni kuwa, magari waliyokabidhiwa yatakuwa nyenzo muhimu kwa viongozi wakiwemo Makatibu Wasaidizi wa Wilaya katika usimamizi na ufuatiliaji wa Elimu nchini ikiwa ni pamoja na utatuzi wa kero zinazojitokeza.

Aidha, Waziri alielekeza kuwa magari hayo yatunzwe vizuri ili kuweza kuongeza ufanisi na ubora wa elimu katika utekelezaji wa majukumu ya kuwahudumia walimu ili wapite salama katika mzunguko wao wa ajira.

Mhe. Mchengerwa alisema kuwa baada ya kupata magari hayo hakutakuwa na visingizio vya kushindwa kutembelea walimu katika kusikiliza na kutatua changamoto zao badala ya kuwasubiri wawafuate ofisini.

Aidha, Mhe. Mchengerwa alisema kuwa kwa ofisi za Tume ambazo hazijapata magari, zinatakiwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika kuwafikia walimu kwa kutumia vitendeakazi vilivyopo pamoja

na kushirikiana na Wakurugenzi wa Halmashauri katika maeneo yao ili walimu waendeleo kupata huduma bora.

“Nimeshaelekeza na leo ninarudia tena kuelekeza Wakurugenzi wa Halmashauri zote nchini kuhakikisha wanaweka mazingira mazuri kwa watumishi wa TSC waliopo katika maeneo yao ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Pale wanapohitaji kuwafikiwa walimu, wakurugenzi wawapatie magari ili kazi za TSC zisikwame. Katibu Mkuu hakikisha hotuba yangu inawafikiwa wakurugenzi wote nchini ili agizo hilo litekelezwe kikamilifu,” alisema Waziri Mchengerwa.

Mhe. Mchengerwa aliwaagiza viongozi waliokabidhiwa magari kuhakikisha yanatumika kwa kuzingatia miongozo ya Serikali na kuyatunza ili yadumu.

Magari hayo yamenunuliwa chini ya Mradi wa BOOST ambapo Ofisi za Wilaya zilizopata Magari hayo ni Ilala, Tanga, Mbeya, Nyamagana, Rufiji, Kaliua, Bukombe, Kilosa na Ruangwa huku gari moja (1) ikitumika Ofisi za TSC Makao Makuu.

WAZIRI MCHENGERWA AKABIDHI MAGARI 10 TSC, 9 YAPELEKWA OFISI ZA WILAYA



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Tarwala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Bw. Adolf H. Ndunguru akitoa neno la kumkaribisha Waziri wa Ofisi hiyo, Mhe. Mohamed Mchengerwa wakati wa hafla ya kukabidhi magari kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 Mtumba jijini Dodoma.



Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Tarwala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI), Dkt. Charles Msonde akitoa neno la utangulizi wakati wa hafla ya kukabidhi magari kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 Mtumba jijini Dodoma.



Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Huruma Mageni akitoa neno la shukrani kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI (hayupo pichani) kwa niaba ya Mwenyekiti wa TSC wakati wa hafla ya kukabidhi magari kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 Mtumba jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akiwa katika hafla ya kukabidhi magari kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 Mtumba jijini Dodoma. Pembeni yake ni Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bw. Huruma Mageni.



Kaimu Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (mstari wa mbele) ambao ofisi zao zimepatizwa magari wakizwa katika hafla ya kukabidhi magari kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 Mtumba jijini Dodoma



Baadhi ya Washiriki waliohudhuria hafla kukabidhi magari kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 Mtumba jijini Dodoma wakiwa katika hali ya utulivu wakati wa hafla hiyo.

WAZIRI MCHENGERWA AKABIDHI MAGARI 10 TSC, 9 YAPELEKWA OFISI ZA WILAYA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa akikabidhi funguo za gari kwa mmoja wa Kaimu Katibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu ambao ofisi zao zimepata magari.



Baadhi ya Washiriki waliohudhuria hafla kukabidhi magari kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 Mtumba jijini Dodoma wakiwa katika haliya utulivu wakati wa hafla hiyo.



Baadhi ya magari yaliokabidhiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Mohamed Mchengerwa kwa Kaimu Katibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu katika hafla iliyofanyika tarehe 11 Agosti, 2024 Mtumba jijini Dodoma.

WAJUMBE TENGENI MUDA KUTEMBELEA OFISI ZA TSC ZILIZOPO KATIKA MAENEO YENU: PROF MURUKE



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Muruke akiongoza Mkutano wa TSC tarehe 28 Agosti, 2024 mjini Morogoro. Pichani, kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.

Na Mwandishi Wetu - TSC, Morogoro

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Muruke ametoa wito kwa Wajumbe wa TSC kutembelea ofisi za Tume hiyo ngazi ya Wilaya zilizopo karibu na maeneo yao

kwa lengo la kupata maoni na kufahamu changamoto zinazowakabili watumishi katika maeneo hayo.

Prof. Muruke ametoa kauli hiyo tarehe 28 Agosti, 2024 wakati akiendesha Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu unaofanyika mjini Morogoro.

Alisema kuwa Wajumbe wa Tume wana wajibu wa kusimamia

na kuhakikisha Ofisi zote za TSC zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu katika kutoa huduma kwa walimu.

"Mimi mwenyewe jana niliona ni vema kutembelea Ofisi za Tume Wilaya ya Morogoro kwa kuwa nipo hapa Morogoro. Tukitembelea ofisi zetu hizi tunapata fursa ya kufahamu mazingira ya kazi ambayo wenzetu wanafanyia kazi. Pia, inasaidia kupata maoni yao na kufahamu changamoto zinazoweza kukwamisha utoaji wa huduma bora kwa walimu," alisema.

Aliongeza kwa kusema kuwa, "kwa kutembelea ofisi zetu, inatusaidia kuwa katika mazingira mazuri ya kufanya maamuzi sahihi kwa maslahi ya maendeleo ya walimu."

Prof. Muruke aliwaeleza Wajumbe hao kuwa wanaweza kutembelea ofisi hizo bila kutumia gharama kubwa hususan kwa ofisi zilizo karibu na maeneo yao au pale wanapokuwa na ziara binafsi au za kazi kupitia ofisi wanazofanyia kazi.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Mwl. Paulina Nkwama akitoa heshima zake za mwisho kwa marehemu Julius Mathew Ndumbaro mara baada ya Misa iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Kiwanja cha Ndege jijini Dodoma kabla kusafirishwa kuelekea mkoani Ruvuma kwa mazishi.

WAJUMBE TENGENI MUDA KUTEMBELEA OFISI ZA TSC ZILIZOPO KATIKA MAENEO YENU: PROF MURUKE



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Muruke (Katikati) akiongoza Mkutano wa TSC tarehe 28 Agosti, 2024 mjini Morogoro. Pichani, kulia ni Makamu Mwenyekiti wa TSC, Bi. Bahati Mgongolwa na kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.



Baadhi ya Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu (mstari wa mbele) wakiwa kwenye Mkutano wa Tume hiyo tarehe 28 Agosti, 2024 mjini Morogoro.



Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ukiwa unaendelea mjini Morogoro tarehe 28 Agosti, 2024.

DKT. DUGANGE AIPONGEZA TSC KWA KUSIMAMIA MAADILI NA MAENDELEO YA WALIMU



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Dkt. Festo Dugange akizungumza wakati alipotembelea Banda la OR – TAMISEMI na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye Maonesho ya Nanenane yanayofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma tarehe 04 Agosti, 2024.

Na Mwandishi wetu – Dodoma.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Dkt. Festo Dugange ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kusimamia kikamilifu masuala ya ajira, nidhamu na maendeleo ya walimu jambo linalofanya walimu kuendelea kutekeleza majukumu

yao kwa utulivu.

Mhe. Dugange ametoa kauli hiyo tarehe 4 Agosti, 2024 alipotembelea banda la TSC katika Maoneshoya Wakulima na Wafugaji (Nanenane) yanayofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.

Amesema kuwa Walimu ni kundi muhimu kutokana na jukumu kubwa walilionalo la kuwatengeneza watoto/wanafunzi

kuwa raia wema wanaoweza kulisaidia Taifa kupiga hatua kimaendeleo.

Alisema viwango vya ufaulu kwa wanafunzi vimeendelea kuongezeka jambo linaloonesha kuwa walimu wanatekeleza wajibu wao wa kufundisha wanafunzi kama inavyotakiwa ikiwa pia ni matokeo ya TSC kuhakikisha maslahi na maadili ya walimu yanazingatiwa.

Pia, ameitaka TSC kuendelea kuongeza juhudi katika kutatua changamoto za walimu hususan katika masuala ya upandishaji vyeo, ubadilishaji wa kazi/cheo kwa wale waliojiendeleza pamoja na haki zingine ambazo walimu wanapaswa kupata kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Katika hatua nyingine Dkt. Dugange amehimiza wananchi kujitokeza kupiga kura kuchagua viongozi wa Serikali za Mitaa kwa kuwa viongozi hao ndio wanaomsaidia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuleta maendeleo katika maeneo yao.

Vilevile, amewataka viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kukitumia Chuo cha Serikali za Mitaa kutoa mafunzo kwa viongozi watakoachaguliwa katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba 2024 na wale watakoachaguliwa katika Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba 2025 ili waweze kutimiza majukumu yao ipasavyo.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Mhe. Dkt. Festo Dugange akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Idaraya Tawala za Mikoa sehemu ya Uchumi na Uratibu wa Sekta za Uzalishaji wa OR – TAMISEMI, Bw. Enock Nyanda wakati alipotembelea Banda la OR – TAMISEMI na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye Maonesho ya Nanenane yanayofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma tarehe 04 Agosti, 2024.



DKT. DUGANGE AIPONGEZA TSC KWA KUSIMAMIA MAADILI NA MAENDELEO YA WALIMU



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – AMISEMI), Mhe. Dkt. Festo Dugange akizungumza wakati alipotembelea Banda la OR – TAMISEMI na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye Maonesho ya Nanenane yanayofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma tarehe 04 Agosti, 2024.



Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – AMISEMI), Mhe. Dkt. Festo Dugange akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Idaraya Tawala za Mikoa sehemu ya Uchumi na Uratibu wa Sekta za Uzalishaji wa OR – TAMISEMI, Bw. Enock Nyanda wakati alipotembelea Banda la OR – TAMISEMI na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye Maonesho ya Nanenane yanayofanyika Kitaifa katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma tarehe 04 Agosti, 2024.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Bw. Adolf Ndunguru akimkaribisha Naibu Katibu Mkuu (afya) wa OR–TAMISEMI, Dkt. Grace E. Magembe mara baada ya kuteuliwa na kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nafasi hiyo hivi karibuni.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) (Elimu), Bw. Atupele W. Mwambene (wa kwanza kushoto) na Naibu Katibu Mkuu (afya) wa OR – TAMISEMI, Dkt. Grace E. Magembe (wa pili kutoka kushoto) wakipokelewa na viongozi na watumishi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI mara baada ya kuteuliwa na kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushika nafasi hizo hivi karibuni.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI), Bw. Adolf Ndunguru akiwatambulisha watumishi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa Naibu MaKatibu Wakuu wa Ofisi hiyo, Dkt. Grace Magembe (afya) na Bw. Atupele W. Mwambene (Elimu) walipowasili OR - TAMISEMI Mtumba jijini Dodoma mara baada ya kuteuliwa na kuapishwa kushika nafasi hizo.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa pamoja na viongozi wengine wa Ofisi ya Rais TAMISEMI wakati wa hafa ya kuwvapoeka Naibu Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Grace Magembe (afya) na Bw. Atupele W. Mwambene (Elimu) iliyofanyika katika Ofisi za TAMISEMI Mtumba jijini Dodoma.



Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Bw. Adolf Ndunguru (wa kwanza kushoto mstari wa mbele) akiwa katika picha ya pamoja na Naibu Makatibu Wakuu Ofisi ya Rais TAMISEMI (mstari wa mbele) pamoja na viongozi na watumishi mbalimbali wa Ofisi ya Rais TAMISEMI wakati wa hafla ya kuwvakaribisha Naibu Makatibu Wakuu wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Dkt. Grace Magembe (afya) na Bw. Atupele W. Mwambene (Elimu) iliyofanyika katika Ofisi za TAMISEMI Mtumba jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akizungumza katika banda la Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) tarehe 6 Agosti 2024 katika Maonesho ya Nananane jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akiwa katika mahojiano na waandishi wa habari (hawapo pichani) alipotembelea Maonesho ya Nananane jijini Dodoma tarehe 6 Agosti 2024.

Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi Stella Chimela akitoa ufafanuzi kuhusu masuala ya utumishi wa walimu kwa wateja waliotembelea banda la TSC katika Maonesho ya Nananane jijini Dodoma.



Wanafunzi wakipata maelezo kutoka kwa Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwenye Maonesho ya Nananane katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama akipitia hoja mbalimbali zilizoibuliwa na wateja waliotembelea banda la TSC kwenye Maonesho ya Nanenane jijini Dodoma.

Wanafunzi wakipata maelezo kutoka kwa Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwenye maonesho ya Nanenane katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma.



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wanaotoa huduma kwenye maonesho ya Nanenane katika Viwanja vya Nzuguni jijini Dodoma wakiwa katika picha ya pamoja.

TSC IMEFANIKIWA KUUNGANISHA MFUMO WA TSCMIS NA MIFUMO MINGINE MITATU



Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Takwimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Bi. Kainda Ndasu akitoa mada kuhusu wasilisho la mfumo wa kielektroniki wa Tume ya Utumishi wa Walimu kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wapya wa Tume yalifanyika Morogoro hivi karibuni.

Na Mwandishi wetu -TSC, Morogoro

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), imefanikiwa kuunganisha Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za walimu (TSCMIS) kwa ajili ya kusomana na Mifumo mingine ili iweze kubadilishana taarifa muhimu za walimu.

Kauli hiyo imetolewa hivi karibuni na Mkuu wa Kitengo cha Teknolojia ya Habari, Mawasiliano na Takwimu kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi. Kainda Ndasu wakati akitoa mada kuhusu wasilisho la mfumo wa kielektroniki wa Tume ya Utumishi

wa Walimu (TSC) kwenye mafunzo ya kuwajengea uwezo wajumbe wapya wa Tume hiyo yaliyofanyika mjini Morogoro.

Alisema kuwa Mfumo wa TSCMIS hivi sasa umeunganishwa na Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi (e -watumishi), Mfumo wa Malipo ya Pensheni (Treasury Pensioners Payment System) na Mfumo wa Taarifa za Shule (School Information System) ambao utawezesha kujua mahudhurio, vipindi vinavyofundishwa na shule zenyewe.

Bi. Kainda alisema kuwa lengo la kuunganisha mifumo hiyo ni kutaka kubadilishana taarifa muhimu za walimu na kuboresha

utendaji kazi, kuwa na taarifa sahihi katika kushughulikia masuala ya Ajira, Nidhamu, Rufaa na Mafao kwa walimu.

Bi. Kainda alisema kuwa Mfumo huo umesaidia kuboresha utekelezaji wa majukumu katika kuwahudumia walimu kwa wakati na kwa ufanisi, kurahisisha mchakato wa kushughulikia mashauri ya Nidhamu na Rufaa za walimu kuanzia ngazi ya Shule, Wilaya hadi Makao Makuu na kurahisisha zoezi la kutoa namba za usajili kwa walimu (TSC Number).

Aliongeza kuwa Mfumo huo unawasaidia Walimu kupata huduma wakiwa katika vituo vya kazi na kuwaondolea usumbufu wa kufuata huduma katika Ofisi za Tume ngazi ya wilaya na upatikanaji wa taarifa kwa wakati na kwa usahihi.

Aidha, Bi. Kainda alisema kuwa Tume imepanga kuendelea na awamu ya tatu (3) ya ujenzi wa Mfumo wa TSCMIS pamoja na kufanya maboresho zaidi kulingana na mahitaji ya watumiaji hususan uchakataji wa taarifa kwa ajili ya maamuzi mbalimbali, kuendelea na usimikaji wa miundombinu ya mtandao wa intaneti kwenye Ofisi 103 za wilaya; na kutoa mafunzo kwa watumishi wa Tume katika Mikoa 15, Wakuu wa Shule na Maafisa TEHAMA wa Halmashauri.

Katika hatua nyingine alisema kuwa Tume imetoa mafunzo kwa watumishi 65 kutoka Ofisi za Makao Makuu na Wilaya kwenye Mikoa minne (4); Dar es salaam, Dodoma, Mwanza, Iringa, Wilaya ya Kishapu na Morogoro katika awamu ya kwanza.

Aliongeza kuwa jumla ya watumishi 86 wa Ofisi za wilaya katika Mikoa saba (7), Katavi, Rukwa, Kigoma, Pwani, Singida, Simiyu na Mara wamepata mafunzo katika awamu ya pili kupitia ufadhili wa SHULEBORA.



Picha mbalimbali za wateja na watoa huduma katika banda la Ofisi ya Rais Tamisemi pamoja na Taasisi zake ikiwemo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Viwanjwa vya Nzuguni jijini Dodoma mapema mwezi Agosti, 2024.

PROF. MURUKE AWAPONGEZA WATUMISHI WA TSC WILAYA YA MOROGORO KWA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Prof. Masoud Muruke (kushoto) akisaini kitabu cha wageni wakati ziara yake kwenye Ofisi Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Morogoro iliyoifanyika tarehe 27 Agosti, 2024.

Na Mwandishi Wetu -TSC, Morogoro

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Muruke tarehe 27 Agosti, 2024 ametembelea Ofisi za TSC Wilaya ya Morogoro na kuwapongeza watumishi wa Wilaya hiyo kwa namna wanavyotekeleza majykumu yao katika kutoa huduma kwa walimu.

Akitoka pongezi kwa Watumishi wa TSC wa Wilaya hiyo, Prof. Muruke alisema kuwa licha ya changamoto mbalimbali zinazokabili ofisi hiyo, watumishi hao wameendelea kutekeleza majukumu yao kwa bidii, weledi na uzalendo na hivyo kufanya walimu wa Wilaya hiyo kuendelea kupata huduma bora.

Pamoja na pongezi hizo, Mwenyekiti huyo aliwataka watumishi hao kuendelea kutoa huduma bora kwa walimu ambao

ni watumishi muhimu katika kuzalisha kada mbalimbali ambazo zinahitaji kwa maendeleo ya Taifa.

Prof. Muruke alisema kuwa alipokuwa ziarani Mkoani Dar es Salaam alifurahishwa na uchapakazi mzuri aliuona kwa Watumishi wa Tume wa wilaya za Mkoa huo na kuwataka kuendelea kutoa huduma bora licha ya kuwa na changamoto mbalimbali zinazowakabili ikiwemo uhaba wa miundombinu ya ofisi.

Aidha, Mwenyekiti aliitaka Menejimenti ya TSC kuhakikisha inaendelea kuboresha mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa Ofisi zake za wilaya kwani zenyewe ndio shina la kuleta mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Prof. Muruke aliongeza kuwa ni vema kuimarisha Ofisi za Wilaya ikiwemo kuwa na mazingira mazuri ya kuhifadha nyaraka ambapo wakati mwingine zinatumiwa katika utoaji maamuzi ya masuala mbalimbali yanayohusu utumishi

wa walimu.

"Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) inagusa sehemu kubwa ya utumishi wa walimu ikiwemo ajira, maendeleo ya walimu na inatoa maamuzi yanayohusu nidhamu za walimu, hivyo ni vyema tuhakikishe tunaweka mazingira mazuri ya katika ofisi hizi ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi," alisema.

Naye Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama amewataka Watumishi wa Tume wilayani Morogoro kuhakikisha wanakwenda kutoa huduma kwa walimu katika maeneo yote ya Wilaya hiyo yakiwemo maeneo ya pembezoni kama Mvuhu na Matombo.

Alisema kuwa maeneo ya Mvuhu na Matombo yako mbali na ofisi za TSC, hivyo ni vyema kwa watumishi wa Tume kuweka utaratibu wa kupangiana zamu (rotation) ya kuwafikishia huduma walimu katika maeneo hayo.

PROF. MURUKE AWAPONGEZA WATUMISHI WA TSC WILAYA YA MOROGORO KWA KUTOA HUDUMA BORA KWA WALIMU



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Prof. Masoud Muruke (kushoto) akisaini kitabu cha wageni wakati wa ziara yake kwenye Ofisi Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Morogoro iliyofanyika tarehe 27 Agosti, 2024.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (kulia) akitoa ufafanuzi wakati wa alipoongozana na Mwenyekiti wa TSC kutembelea Ofisi ya Tume Wilaya ya Morogoro tarehe 27 Agosti, 2024.

Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Morogoro, Bi. Rabia Ngairo (wa pili kutoka kushoto) akitoa maelezo kwa Mwenyekiti wa TSC, Prof. Masoud Muruke (wa kwanza kushoto) alipotembelea Ofisi hiyo tarehe 27 Agosti, 2024. Pichani, wa kwanza kutoka kulia ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Muruke (wa tatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa TSC Wilaya ya Morogoro wakati wa ziara yake kwenye Ofisi iliyofanyika tarehe 27 Agosti, 2024. Pichani, wa nne kutoka kulia ni Katibu wa Tume TSC, Mwl. Paulina Nkwama.



Picha mbalimbali za wateja na watoa huduma katika banda la Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Taasisi zake ikiwemo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Vivanjwa vya Nzuguni jijini Dodoma mapema mwezi Agosti, 2024.

WANANCHI WAOMBA SERIKALI KUBADILI SHERIA ILI TSC IWEZE KUTOA HUDUMA KWA WALIMU WA SHULE ZA UMMA NA BINAFSI

**Na Mwandishi Wetu -
TSC-DODOMA**

Baadhi ya wananchi waliotembelea banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wameiomba Serikali kuifanyia mabadiliko Sheria iliyoanzisha Tume hiyo ili iweze kuwahudumia Walimu waliopo katika Shule za Serikali na wale wanaofundisha shule binafsi.

Ombi hilo limetolewa Tarehe 3 Agosti, 2024 na Bw. Ndaji Mayige wakati alipotembelea Banda la Maonesho la Tume ya Utumishi wa Walimu katika Viwanja vya Nzunguni jijini Dodoma ambapo ndipo maonesho ya Kitaifa yalipofanyika.

Alisema kuwa walimu wote wanatoa huduma kwa watoto wote wa kitanzania ni vema wakawa na chombo kimoja kinachosimamia nidhamu na maadili yao wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

"Hatua hii ni muhimu kwa kuwa pindi Mwalimu anapokiuka maadili na kuchukuliwa hatua hawezi kuwa na sehemu ya kukimbilia kwa kuwa taarifa zake zitakuwa katika chombo kinachowasimia wote...kwani ilivyo sasa Mwalimu akikiuka maadili na kuchukuliwa hatua ikiwemo kufukuzwa anaweza kukimbilia shule nyingine za binafsi na kuendelea kufundisha wakati amepatikana na hatia," alisema.

Wakati huo huo ameiomba Serikali kurudisha mtihani wa mchujo wa wanafunzi wanaokuwa wamechaguliwa kujiunga na vyuo vya ualimu kabla ya kujiunga ili kupata wanachuo ambao watakuwa mahiri kwa ajili ya kutengeneza wataalamu wajao.

Katika hatua nyingine Bw. Daniel Kayanda aliomba Serikali



Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Bi. Stella Chimela (kushoto) na Mtumishi wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo wakimsikiliza mwananchi aliyetembelea maonesho ya nane nane jijini Dodoma.

kuboresha mwongozo wa Taasisi binafsi ili haki za watumishi wanaotoa huduma ili ziwe sawa kote nchini ikiwemo kuweka mishahara inayofanana kwa kuondoa tofauti kwa walimu walioanza kazi muda mmoja.

Kwa upande wa Dkt. Didas

Malale ameipongeza TSC kwa kushughulikia maslahi ya watumishi (walimu) hasa katika suala la kuwapandisha vyeo kwa kutumia utaratibu mzuri ukilinganisha na kipindi kilichopita.

WANANCHI WAOMBA SERIKALI KUBADILI SHERIA ILI TSC IWEZE KUTOA HUDUMA KWA WALIMU WA UMMA NA SHULE BINAFSI



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakitoa huduma kwa wananchi waliotembelea maonesho ya nane nane Kitaifa jijini Dodoma.

Mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Bi. Stella Chimela (kushoto) na Mtumishi wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo wakimsikiliza mwananchi aliyetembelea maonesho ya nane nane jijini Dodoma.



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakitoa huduma kwa wananchi waliotembelea maonesho ya nane nane Kitaifa jijini Dodoma.



Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala, Fedha, Utafiti na Elimu kwa Umma ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi Mariam Gerald Mwanikwa akiwasilisha taarifa ya Kamati yake kwenye Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 28 Agosti, 2024 mjini Morogoro.



Mwenyekiti wa Kamati ya Ajira na Maendeleo ya Walimu ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi Hadija Mcheka akiwasilisha taarifa ya Kamati yake kwenye Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 28 Agosti, 2024 mjini Morogoro.



Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi Jane Mtindya akiwasilisha taarifa ya Kamati yake kwenye Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu tarehe 28 Agosti, 2024 mjini Morogoro.



Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Masoud Muruke (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakati wa Mkutano wa Tume mjini Morogoro tarehe 28 Agosti 2024. Pichani, wa pili kutoka kushoto ni Katibu wa TSC, Mwl. Paulina Nkwama.



Picha mbalimbali za wateja na watoa huduma katika banda la Ofisi ya Rais Tamisemi pamoja na Taasisi zake ikiwemo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Vivanjwa vya Nzuguni jijini Dodoma mapema mwezi Agosti, 2024.



Picha mbalimbali za wateja na watoa huduma katika banda la Ofisi ya Rais Tamisemi pamoja na Taasisi zake ikiwemo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Vivanjwa vya Nzuguni jijini Dodoma mapema mwezi Agosti, 2024.



Picha mbalimbali za wateja na watoa huduma katika banda la Ofisi ya Rais Tamiseemi pamoja na Taasisi zake ikiwemo Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakati wa Maonesho ya Nanenane yaliyofanyika katika Vizwanjwa vya Nzuguni jijini Dodoma mapema mwezi Agosti, 2024.

MENEJIMENTI YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YATAKIWA KUFANYA UTAFITI KUBAINI CHANZO CHA MAKOSA YA WALIMU

**Na Mwandishi wetu –
TSC, Morogoro**

Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeagizwa kufanya utafiti kubaini chanzo cha makosa ambayo yanawakumba walimu na kuwasababishia kuadhibiwa.

Kauli hiyo imetolewa na Kamishna Mariam Mwanilwa akitoa maoni yake kabla ya kufungwa kwa mkutano wa siku tatu wa Tume hiyo uliolenga kuamua masuala mbalimbali ikiwemo rufaa za walimu.

Kamishna Mariam Mwanilwa alisema kuwa katika kipindi cha siku tatu wamesikiliza na kutoa uamuzi wa jumla ya rufaa 16 ambapo 6 waliwaliomba kufika mbele ya Tume kwa ajili ya kuongeza maelezo katika utetezi wao wa maandishi na rufaa ziliwasilishwa kwa njia ya maandishi.

Alisema kuwa katika idadi hiyo walimu waliozaliwa kati ya mwaka 1980 hadi 1988 waliongoza kwa kutuhumiwa kwa kuwa na walimu 11, waliozaliwa kati ya 1971-1979 walikuwa ni wawili na mwaka 1990-1992 walikuwa 2.

Alisema kuwa kwa kuangalia takwimu hizo ufanyike utafiti kuangalia aina ya makosa, umri na jinsi ambayo walimu wamekuwa wakituhumiwa kuyafanya zaidi.

Aidha, Kamishna huyo alishauri kuongeza nguvu zaidi katika kutoa elimu kwa walimu kuhusu masuala mbalimbali yakiwemo ya nidhamu ili kuwaepusha kufanya makosa ambayo yanasababisha baadhi yao kufukuzwa kazi.

Naye Kamishna Jane Mtindya



Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bi. Bahati Mgongolwa akitoa neno la kufunga Mkutano wa Tume tarehe 30 Agosti 2024 mjini Morogoro.



Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi Mariam Gerald Mwanilwa akichangia hoja wakati wa kuelekea kuahirishwa kwa Mkutano huo tarehe 30 Agosti, 2024 mjini Morogoro.

alisema kuwa hatua hiyo ya kufanya utafiti ni ya msingi kwani hata miaka ya nyuma walishaagiza kufanyika ambapo ilibainika kuwa vijana wengi waliozaliwa miaka ya 1990 waliamua kusomea Kada ya Ualimu kwa lengo la kupata

mikopo ya elimu ya juu iliyokuwa ikitolewa na Serikali.

Kamishna Jane aliongeza kuwa utafiti huo utawezesha Serikali kuchukua hatua stahiki kusaidia kutatua changamoto hiyo.

MENEJIMENTI YA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU YATAKIWA KUFANYA UTAFITI KUBAINI CHANZO CHA MAKOSA YA WALIMU



Baadhi ya Makamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wakifuatilia mjadala wakati wa Mkutano huo uliohitimishwa tarehe 30 Agosti, 2024 mjini Morogoro.




Mkurugenzi wa Huduma za Sheria wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Wakili Richard Odongo akionesha jambo wakati wa Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu uliofanyika mjini Morogoro na kuhitimishwa tarehe 30 Agosti, 2024.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu